**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/CZ/2024/05**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000228**

**EVA LUDGER KOMBA ............................................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA DODOMA (DUWASA) ............................................ MLALAMIKIWA**

---

# AMRI

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA leo tarehe 28 mwezi wa Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 28 mwezi wa Februari 2025 kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe kumpatia huduma ya maji katika makazi yake angalau mara tatu (3) kwa wiki kwani anaamini Mlalamikiwa anao uwezo wa kufanya hivyo, kwakuwa baadhi ya majirani zake wanapata huduma hiyo.

Mlalamikaji aliwasilisha Malalamiko yake EWURA mnamo tarehe 10 Oktoba 2024. Mlalamikiwa akaelekezwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)). Mnamo tarehe 05 Novemba 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na

kuieleza Mamlaka kwamba Mlalamikiwa anakiri kupokea malalamiko haya na alieleza kwamba jitihada zinazofanywa na Mlalamikiwa kuhakikisha Mlalamkikaji anapata huduma ya maji safi kwa kadiri itakavyowezekana. Mlalamikiwa aliendelea kueleza kwamba katika jitihada hizo, Mlalamikiwa alishatoa mipango yote ya suluhu ya tatizo hilo kwa kupitia barua yao waliomjibu Mlalamikaji ya tarehe 27 Septemba 2024.

Vikao vya usuluhishi baina ya pande zote mbili vilifanyika tarehe 28 Novemba 2024 na 23 Disemba 2024 katika ukumbi wa Ofisi za EWURA Kanda ya Kati, Jengo la EWURA, Ghorofa ya kwanza uliopo Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma. Mwisho wa kikao cha usuluhishi na Wadaawa walikubaliana kupeana muda kwa Mlalamikiwa kufanya marekebisho ya miundombinu yake na kupelekea Mlalamikaji kupata huduma ya maji. Tarehe 4 Februari 2025 Mlalamikaji aliandika barua pepe ya kuondoa Shauri hili kwa kuwa Mlalamikiwa ameshatatua changamoto yake na maji kwa sasa yanapatikana. Hivyo, Mlalamikaji anaomba kuondoa malalamiko yake EWURA.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama zake za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 28 mwezi wa Februari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**